

# Mabadiliko Muhimu kwa Sheria ya Viti vya Gari ya Vermont

Ilianza kutumika tarehe 1 Julai 2024

Sheria ya Viti vya Gari ya Vermont (23 VSA § 1258) imeboreshwa ili kulingana zaidi na mapendekezo ya Chuo cha Madaktari wa Watoto cha Marekani (American Academy of Pediatrics, AAP). Kila hatua inatoa ulinzi mdogo kuliko hatua ya awali. Weka mtoto wako katika kila hatua kwa muda mrefu iwezekanavyo.

## Haya Ndio Unahitaji Kujua:

### Kuzaliwa hadi Miaka 2



Watoto chini ya umri wa miaka miwili lazima wawekwe ipasavyo kwenye kiti cha gari cha watoto kinachoangalia nyuma chenye lijamu kilichoidhinishwa na serikali kuu.

Mtoto aliye katika kiti cha gari kinachoangalia nyuma hapaswi kuketi mbele ya mfuko wa hewa.

### Miaka 2 hadi 5



Watoto wenye umri wa zaidi ya miaka miwili lakini hawajafikisha miaka tano, wanapaswa kuwekwa kwenye kiti kinachoangalia nyuma au kiti kinachoangalia mbele chenye lijamu kilichoidhinishwa na serikali kuu.

### Miaka 5 hadi 8



Watoto chini ya umri wa miaka nane ambao hawajawekwa kwenye kiti cha gari chenye lijamu wanapaswa kuwekwa ipasavyo katika kiti cha nyongeza.

### Zaidi ya 8



Watoto chini ya umri wa miaka 18 ambao hawajawekwa kwenye kiti cha gari chenye lijamu au kiti cha nyongeza lazima wafunge mkanda wa kiti.

Watoto chini ya umri wa miaka 13 lazima, ikiwa inawezekana, wakae kwenye kiti cha nyuma.

## Vikumbusho Muhimu kwa Kila Mtu:

- Watoto wanapaswa kuketi kwenye kiti cha nyuma hadi wafikie umri wa miaka 13.
- Daima funga mkanda ili kuwa salama na kuwa mfano mwema.
- Daima rejelea maagizo ya watengenezaji wa kiti chako cha gari na gari lako ili kuhakikisha kiti cha mtoto wako kimewekwa na kinatumika kwa usahihi.



Kwa maelezo zaidi au kupata kituo chako cha msaada wa kiti cha gari, tembelea [www.BeSeatSmart.org](http://www.BeSeatSmart.org)

Oktoaba 2024